Afisi ya Habari
ya Hizb ut Tahrir
Wilayah Sudan

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Hizb ut Tahrir

**Jumapili, 5 Muharram 1445 H** | **23/07/2023 M** | **Na: HTS 1445 / 02**

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari
## Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Sudan Wakutana na Mkuu wa Kabila la Bakr
## (Imetafsiriwa)

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Wilayah Ya Sudan ukiongozwa na Ustadh Muhammad al-Hassan Ahmad, Mwanachama wa Baraza la Hizb ut Tahrir katika Wilayah ya Sudan, akiandamana na wanachama wa Hizb Ut Tahrir: Ndugu: Muhammad Mukhtar, Muntasir Karar, na Al-Samad al-Tayyib ulikutana na mkuu wa kabila la Bakr huko Gadharef, Ustadh Saif al-Dawla Haidar al-Taher Bakr, katika Baraza diwan (baraza) yake, kwa uwepo wa Ustadh Muhammad Fadl, mkuu wa Chama cha Kijamhuri huko Gadharef.

Baada ya kufahamiana, ujumbe huo ulifafanua mtazamo wa hizb kuhusu mzozo nchini Sudan, na kwamba sababu kiasili ilitokana na mvutano wa Marekani na Ulaya kwa ajili ya ushawishi nchini Sudan, na uporaji wa utajiri wake kupitia vibaraka wao. Hii ndio sababu mzozo umebakia unatokota kati ya majeshi ya Marekani (Jeshi na Vikosi vya Msaada wa Haraka), na kati ya raia wa Ulaya, na kwamba vita hivi kati ya majeshi kwa kweli kwa ajili ya kuwaondoa wapambe wa Ulaya kutoka kwa mandhari ya kisiasa, au angalau kuzuia nguvu halisi kuwepo mikononi mwao.

Ujumbe huo ulieleza kuwa hakuna suluhisho kwa yale yanayotokea nchini Sudan, au katika nchi zengine za Kiislamu, isipokuwa kwa kusimamisha mfumo wa Kiislamu. Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, na kazi kubwa ya kuzuia vita, na (kulinda) utukufu wa damu ya Waislamu.

Mwisho wa mkutano, ujumbe huo ulimshukuru mkuu huyo kwa ukarimu na mapokezi mazuri.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Sudan**

**Simu:** 0912240143- 0912377707
**Pepe:** Spokman_sd@dbzmail.com
**Tovuti:** www.hizb-sudan.org

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.info